

## WIZARA YA AFYA

### MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA TFDA



### HULINDA AFYA ZA JAMII

#### Utangulizi

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi iliyoko chini ya Wizara ya Afya inayosimamia udhibiti wa ubora wa vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba. TFDA imeanzishwa chini ya sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya mwaka 2003 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Dawa na Sumu Na. 9 ya mwaka 1978 (iliyokuwa inadhibiti ubora na usalama wa dawa na taaluma ya famasia) na sheria ya Udhibiti wa Ubora wa Vyakula Na. 10 ya 1978 (iliyokuwa inadhibiti ubora wa vyakula). Chombo hiki kilianza kutekeleza majukumu yake tangu tarehe 1 Julai 2003.

TFDA imepewa madaraka ya kufanya maamuzi mbalimbali ya kiutendaji kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 na ile ya Wakala za Serikali ya mwaka 1997.

#### Lengo kuu la kuunda TFDA

Mamlaka ya Chakula na Dawa imeundwa ili kulinda afya ya wananchi wote kwa ujumla kwa kuzuia athari ambazo zingeweza kujitokeza kutokana na matumizi ya chakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba.

#### Dira

Kuwa taasisi bora zaidi katika utoaji wa huduma za udhibiti wa vyakula, dawa vipodozi na vifaa tiba miongoni mwa nchi za Africa zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara kabla ya mwaka 2010.

#### Kazi za TFDA

1. Kusajili, kufanya ukaguzi, kupima ubora, kusimamia utengenezaji, ufungaji, uingizaji nchini na uuzaji wa vyakula ili kuhakikisha mwananchi anapata vyakula bora na salama. Pia kuhakikisha usafi wa machinjio na uuzaji wa nyama
2. Kudhibiti utengenezaji, uingizaji nchini, usambazaji, uuzaji, na usafirishaji nje ya nchi wa dawa za binadamu na mifugo
3. Kusimamia majaribio ya dawa mpya na vifaa tiba (*clinical trials*)

4. Kudhibiti utengenezaji, uingizaji nchini, usambazaji na uuzaji wa vipodozi; kudhibiti matumizi ya kemikali hatari ambazo huchanganywa katika vipodozi; kudhibiti matumizi mabaya ya dawa zinazotumika kama vipodozi.
5. Kudhibiti ufungaji, uwekaji vielelezo na ubora wa vyombo au vifaa vitumikavyo kufungashia vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba.
6. Kudhibiti utoaji wa matangazo ya vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba ili kumlinda mtumiaji dhidi ya matangazo ambayo si sahihi na hayaendani na hali halisi au ukweli kuhusu usalama na ubora wa bidhaa hizo
7. Kutoa taarifa na kuelimisha jamii kuhusu ubora, usalama na matumizi sahihi ya vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba
8. Kuratibu madhara yatokanayo na utumiaji wa vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba

## Muundo wa TFDA

TFDA inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye anawajibika kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na

Ustawi wa Jamii. **\*Mkurugenzi Mkuu anasimamia masuala yote ya kiutendaji ya Mamlaka.** Chini ya Mkurugenzi Mkuu kuna Kurugenzi nne:

**Kurugenzi ya Uendeshaji Huduma-** inasimamia utawala, fedha, elimu kwa umma, na kuhakikisha shughuli mbali mbali za TFDA zinafanyika kwa ufanisi

**Kurugenzi ya Usajili wa Bidhaa-** hutathmini taarifa mbali mbali za chakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi, na vifaa tiba kabla ya kuidhinishwa kwa matumizi

**Kurugenzi ya Ukaguzi-** hufuatilia na kuchunguza usalama wa vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba. Pia hukagua sehemu zote zinazojihusisha na biashara za bidhaa hizi ili kuhakikisha kama taratibu zinafuatwa

**Kurugenzi ya huduma za maabara-** hupima ubora wa vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba.

\* Ili kuweza kutekeleza majukumu na kazi zake kwa urahisi, Mamlaka inashirikiana na taasisi mbali mbali za serikali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuhakikisha kwamba ukaguzi wa mara kwa mara unafanywa ili kuweza kufuatilia ubora wa bidhaa zilizoko kwenye soko.

## Wadau wa TFDA

- watengenezaji, waingizaji nchini, wasafirishaji nje ya nchi, wasambazaji na wauzaji wa vyakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi, na vifaa tiba
- wasimamiaji wa sheria
- wafanyakazi wa afya na watafiti
- idara za serikali na binafsi
- mashirika ya kimataifa
- mashirika yasiyo ya kiserikali
- vyombo vya habari
- vyama vya walaji
- walaji, watumiaji na wananchi wote kwa ujumla

## **Matarajio**

- Kuwepo na chakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozi na vifaa tiba vyenye ubora unaokubalika katika soko la Tanzania.
- Elimu na taarifa kuhusu chakula, dawa, dawa za mitishamba, vipodozii na vifaa tiba inatolewa kwa wananchi
- Uongozi na utawala bora wa TFDA

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Mamlaka Chakula na Dawa (TFDA)  
EPI-Mabibo External  
S.L.P 77150  
Dar Es salaam  
Tanzania  
SIMU: 255 22 2450751/2450512  
Fax: 255 22 2450793  
Email: [tfda@simbanet.net](mailto:tfda@simbanet.net)